Bibilia ya watoto
Inaleta



Wakati wa kutisha kwa Yesu

Kimeandikwa na: Edward Hughes
Kimeorodheshwa na: Byron Unger; Lazarus
Imerekebishwa na: M. Maillot; Sarah S.
Alastair Paterson
Kimetafsiriwa na: Grace Chepkoech
Kimedhibitishwa na: Bible for Children
www.M1914.org

BFC
PO Box 3
Winnipeg, MB R3C 2G1
Canada

©2022 Bible for Children, Inc.
License: Kuna ruhusa ya kuchapa hadithi hii, lakini bila ya kuuza.

Yesu alipobatizwa, Mungu alizungumza. Akasema, "Huyu ni Mwana Wangu Mpendwa. Nimefurahikiwa kwake." ROHO MTAKATIFU wa Mungu akatua juu yake kama njiwa.

Baadaye, Roho Mtakatifu wa Mungu akamwongoza Yesu hadi nyikani. Yesu alikuwa peke yake.



3

Yesu akafunga kwa siku arobaine. Hii inamaanisha kuwa hakula chochote. Alikuwa na njaa sana.

4

Bibilia inasema kuwa pia kulikuwa na wanyama wa msituni pale.

5

Shetani akaja kumjaribu Yesu. Hapo zamani alikuwa amewajaribu Adamu na Hawa hadi wakakosa kumtii Mungu katika bustani la Edeni. Sasa Yesu alikuwa anajaribiwa.

6

Shetani aliweza kumjaribu hata mwana wa Mungu, Yesu.



7

"Kama wewe ni mwana wa Mungu," shetani akasema, "badilisha mawe haya yawe mkate." Alijua kuwa Yesu alikuwa na njaa. Alijua pia kuwa mwana wa Mungu angeweza kubadilisha mawe kuwa mkate. Je, Yesu angemtii shetani?

8

La! Yesu hakumtii shetani. Badala yake. Alimjibu kutoka kwa neon la Mungu. "Mtu hataishi kwa mkate tu, lakini kwa kila neon litokalo kwa Mungu."



9

Halafu shetani akamwongoza Yesu hadi mji mkuu wa Yerusalemu, hadi hekalu takatifu watu walipokuwa wakimwabudu Mungu. Shetani angefanya nini tena?



10

"Kama wewe ni mwana wa Mungu, jitupe chini," shetani akasema. Neno la Mungu linasema kuwa malaika Wake watakuokoa."



11

"La!" Yesu akamjibu. "Neno la Mungu pia linasema kuwa ... 'Usimjaribu Mungu Bwana wako.'"



12

Shetani akajaribu tena. Akamchukua Yesu nje ya mji hadi juu ya milima.

13

Akamwonyesha Yesu milki zote za ulimwengu. Shetani akasema, "Nitakupa haya yote kama utasujudu mbele yangu na kuniabudu."

14

"Nenda nyuma yangu, shetani!" Yesu akaamuru. "Imeandikwa ... Msujudie Bwana Mungu, umwabudu yeye peke yake.'"



15

Hapo shetani akamwacha Yesu. Halafu kitu cha ajabu kikatendeka. Mungu aliwatuma malaika waje wamhudumie Yesu mwana wake – Ambaye hakutii shetani.



16

Wakati wa kutisha kwa Yesu

Hadithi kutoka kwa Neno la Mungu, Bibilia,

inapatikana katika

Mathayo 4, Luka 4

"Kufafanusha maneno yako kwatia nuru."
Zaburi 119:130

17

Mwisho

I 38 VM 60

18

Hii hadithi ya bibilia inatueleza kumhusu Mungu wetu wa ajabu aliyetuumba na anayetaka tumjue.

Mungu anajua tumetenda mambo mabaya, anayoyaita dhambi. Adhabu ya dhambi ni mauti, lakini Mungu anakupenda sana hata akamtuma mwana wake wa pekee, Yesu, Ili afe msalabani na aadhibiwe kwa dhambi yako. Alafu Yesu akafufuka na kuenda nyumbani mbinguni! Ukimwamini Yesu na kumwomba msamaha kwa dhambi yako, Atakusamehe! Yesu atkuja na kuishi ndani yako, na utaishi naye milele.

Kama unaamini huu ni ukweli, Sema haya kwa Mungu: Mpendwa Yesu, ninaamini kuwa wewe ni Mungu, na ulifanyika mtu ili ufe kwa ajili ya dhambi zangu, ili niwe na maisha mapya, na siku moja nitaenda kuwa nawe millele. Nisaidie nikutii na niishi kwa ajili yako kama mtoto wako. Amina.

Soma bibilia na uzungumze na Mungu kila siku! Yohana 3:16

19